# Muhtasari wa Utafiti

Toleo la: Juni 2022

# Kuendeleza usawa wa jinsia katika  Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii: Mikakati ipi inafaa? Uzoefu kutoka Mradi wa CoForEST

### Ujumbe Muhimu

- ☐ Usawa wa kijinsia unaongeza uhalali na kuleta matokeo yanayotakiwa katika usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii (USMJ).
- ☐ Kuimarisha ushirikishwaji, umiliki ardhi, mgawanyo wa manufaa na utawala kunufaisha wanawake na makundi maalum, ni miongoni mwa mikakati inayofaa kuimarisha usawa wa jinsia katika USMJ.
- ☐ Kama mafunzo kuhusu biashara ya mazao ya misitu yatazingatia jinsia, wanawake wanaweza kunufaika na minyororo ya thamani ya mkaa ambapo wanawake hawajawa washiriki kihistoria.
- ☐ Mchanganyiko wa mikakati unahitajika kuongeza usawa wa jinsia katika USMJ, ikiwa pamoja na mikakati ya kuangalia namna ya kutafuta ufumbuzi wa vyanzo na kupunguza athari hasi za tofauti za kijinsia.

## Jinsia na Usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii

Katika Tanzania, usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii (USMJ) unahusisha ushiriki wa jamii katika kusimamia misitu kwenye ardhi za vijiji. Unapewa nguvu na Sera ya taifa ya Misitu. Mabadiliko ya kijinsia katika USMJ yana akisi yale ya jamii kubwa zaidi. Jinsia inaathiri umiliki na utumiaji wa mazao na huduma za misitukatika USMJ. Kushughulikia tofauti za jinsia katika USMJ kunaongeze ulinzi wa haki za kila mmoja kwa usawa na ni muhimu kama USMJ utachangia maendeleo endelevu. Kupuuzia tofauti za jinsia katika USMJ kunahatarisha kuongezeka kwa udumavu wa usawa na kuondoa uhalali na matokeo tarajiwa ya USMJ.

## Uchambuzi wa mikakati mbalimbali ya kuendeleza USMJ wenye usawa wa kijinsia

Kuna mikakati mbalimbali ambayo watekelezaji wanaweza kutumia kuongeza usawa wa kijinsia katika USMJ. Muhtasari huu wa utafiti unaangalia mikakati kadhaa itakayoshughulikia tofauti za kijinsia katika USMJ ambayo ilikuwa inatumika na Mradi wa Mradi wa kuhifadhi kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST). Lengo la utafiti lilikuwa 'Kuanisha mikakati inayofaa kushughulikia sababu za kiuchumi, kijamii, kitamaduni, kisiasa na za kisheria ambazo zinawapunguzia wanawake na makundi maalum uwezo wa kumiliki na kutumia manufaa ya USMJ.' Utafiti huu ulitumia njia shirikishi zilizojumuisha wanawake na wanamume kutoka

Vijiji tisa vya mradi wa CoForEST kutoka Mkoa wa Morogoro. Mikakati mbalimbali ilichambuliwa kupitia mahojiano ya ana kwa ana na watu maalum, majadiliano ya vikundi, na mipango shirikishi na wadau.

## Matokeo: Mikakati inayofaa kushughulikia tofauti za jinsia katika USMJ

Utafiti ulianisha mikakati mitano iliyoweza kupunguza tofauti za kijinsia katika USMJ.

i. Kuimarisha ushiriki wa wanawake katika Nyanja zote za USMJ pamoja na taasisi kama vile kamati za maliasili za vijiji.
ii. Kuimarisha haki za umiliki wa misitu, ardhi na miti kwa wanawake na makundi maalum.
iii. Usawa katika mgawanyo wa manufaa ya USMJ.
iv. Kuimarisha uwezo wa wanawake kushiriki kwenye mnyororo wa thamani biashara za mazao ya misitu.
v. Kujenga uwezo wa ufahamu na ujuzi wa wanawake na makundi maalum.

Ili kutekeleza mikakati hii, shughuli zifuatazo zibainishwa kufaa zaidi na wanufaikaji wa mradi wa CoForEST:

i. Uhamasishaji wa mara kwa mara kuhusu jinsia na umuhimu wake katika USMJ;
ii. Kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika shughuli za biashara;
iii. Kuwezesha uwundaji wa vikundi tofauti vya wanawake  na wanaume  katika uanzishwaji wa biashara ya mazao ya misitu kama vile mkaa na mbao;
iv. Kuwezesha utekelezaji wa sheria na utawala bora na utekelezaji wa USMJ, ufuataji wa sheria na kiwango cha uvunaji  kwa wajumbe wanawake katika Kamati ya maliasili na kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji.

## Hitimisho

Tofauti za jinsia zimeenea kwenye USMJ  kama vile kwenye: ushirikishwaji, uongozi, haki za kumili ardhi, matumizi ya rasilimali za misitu, mgawanyo wa kazi na wingi wa kazi, utumiaji na umiliki wa mapato, ufikiwaji wa masoko, upatikanaji wa fursa za ajira na ushiriki kwenye utekelezaji na sera. Mikakati ya kufikia usawa wa jinsia unahitaji kushughulikia aina hizi za tofauti zilizopo.

Hatua nyingi zinazochukuliwa kupunguza tofauti za jinsia katika USMJ pia zinapunguza umaskini. Baadhi ya njia zinashughulikia vyanzo vya tofauti za jinsia, wakati nyingine zinapunguza athari za tofauti hizo. Kuongeza uwelewa wa usawa wa jinsia hautoshelezi peke yake. Mchanganyiko wa mikakati unahitajika.

## Kuhusu mradi wa CoForEST

Lengo la mradi wa CoForEST ni kufikia uendelevu ambao utawezesha jamii kusimamia misitu yao kwa njia endelevu na kusababisha mabadiliko ya kiuchumi na utawala bora katika biashara ya minyororo ya thamani ya mazao ya misitu.' Mradi umetekelezwa kwa awamu tatu kati ya mwaka 2012 na 2023 katika vijiji 39 hususan katika Mkoa wa Morogoro, ukanda wa mashariki mwa nchi ya Tanzania.

## Mapendekezo

Kulingana na matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kwamba:

- Mipango ya USMJ iainishe mabadiliko ya jinsia na shughuli za kuendeleza usawa na ushiriki kutoka kwa wanawake na makundi mengine maalum.
- Mikakati na mbinu mbalimbali zitumike kushughulikia vyanzo vikuu vya tofauti za kijinsia,ili kuongeza manufaa ya USMJ kwa wanawake na makundi maalum na kukabiliana na athari hasi.
- Kujenga uwezo wa kuendeleza usawa wa jinsia katika USMJ na kuwezesha jamii kulinda haki za ardhi na rasilimali zinazohitajika kwa wanawake kutoka kwa wawezeshaji na wataalam wa halmashauri.

Kuna haja ya kuhamasisha uundwaji wa kanuni za kukuza usawa wa jinsia katika halmshauri, mashirika, taasisi na vyama vya wazalishaji ili kufungua wigo mpana kwa wanawake katika nafasi za kufanya maamuzi.



*"..nilikuwa nasikia kwamba wanawake wanaweza kujiajiri katika uzalishaji wa mkaa kwa njia endelevu, sikuamini, lakini baada ya kujiunga na mpango wa kuweka na kukopa, niliamua kujiunga na biashara na imeboresha maisha yangu".*

**Muhtasari huu umetokana na: Jeckoniah, J and S. Augustino. 2022. Addressing gender disparities in community-based forest management in Tanzania. TFCG Technical Paper 50.**

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

**Embassy of Switzerland in Tanzania**

http://www.tfcg.org/gender-in-community-based-forest-management-in-tanzania/

Utafiti uliwezeshwa na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi kupitia Mradi wa Mradi wa kuhifadhi kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST).